

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MKOA WA SIMIYU**

**BARIADI**

**KESI YA JINAI NO. 03 YA 2022**

**JAMHURI**

*Dhidi*

**LEVINUS S/O KIDAMABI @ TENGWA ..... .. MTUHUMIWA**

**HUKUMU**

*19 Oktoba 2022*

**M. J Mahumbuga – PRM**

Hii ni hukumu ya Kesi ya Jinai namba 03/2022 ambapo mshitakiwa ambaye ni Levinus s/o Kidamabi @ Tengwa alishtakiwa kwa makosa matatu kama ifuatavyo:-

**Kosa la kwanza:** Uchapishaji wa Taarifa za Uongo C/S 16 ya Sheria ya Uhalifu wa Kimtandao Na. 14 ya 2015.

**Kosa la Pili:** Uchapishaji wa Taarifa za Uongo C/S 16 ya Sheria ya Uhalifu wa Kimtandao Na. 14 ya 2015.

**Kosa la tatu:** Kutosajili laini ya simu iliyokuwa inamilikiwa na mtu mwingine Kinyume na Kanuni ya 4 (1) (c), 12 (3) na 21 (1) ya Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Sim card) Kanuni, 2020 pamoja na kifungu cha 152 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Na. 3 ya 2020.

Maelezo ya kosa hilo yanadaiwa kuwa Desemba 3, 2021 katika Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu , mshitakiwa alichapisha taarifa za uongo kwa njia ya maandishi: " Mzazi mwenzao anawatetea wazazi wenzake , mkiongozwa na mwanamke lazima mtafanywa wote kama mnanyonyesha , Taifa limekuwa kama lina wanawake wote kila siku tunaongelea mambo ya kikekike " na tarehe 4 Disemba, 2021 pia alichapisha habari za uwongo kwa kusema: "Mama yao anakaribia kuugua ukichaa kitaalam tunaita anachokifanya "hallucination" haka kamuungano tufungeni tumuombe Mungu kavunjwe ipo siku hawa watu wakuvuka maji watatuingiza kwemye madeni makubwa maana wanapenda starehe kuliko kazi " katika kundi la WhatsApp linalofahamika kwa jina la SIMIYU BREAKING NEWS kwa nia ya kumkashifu rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mheshimiwa SAMIA SULUHU HASSAN.

Pia ilidaiwa kuwa Desemba 6, 2021 katika eneo la Benki ya NMB Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu , mshtakiwa alikutwa akitumia laini ya simu yenye namba za usajili 0764996612 iliyokuwa ikimilikiwa na Hollo Yonas bila kuisajili kwa njia ya kibayometriki na kumjulisha mtoa huduma mabadiliko ya mtumiaji.

Mshtakiwa alikana mashitaka hayo. Upande wa mashtaka ulileta mashahidi wanne ambao ni E. 5943 Sgt Godfrey, H.7204 DC. Daudi , G.

1730 D/Cpl . Budodi na H. 8174 DC. Iddy na katika kesi hii watajulikana kama PW1, PW2, PW3 na PW4. Kwa upande wa utetezi kulikuwa na mashahidi wawili ambao ni Levinus s/o Kidamabi @ Tengwa na Hollo d/o Yonas @ Jeli na katika kesi hii watatajwa kwa majina ya DW1 na DW2.

Katika ushahidi wa upande wa mshtakiwa mashahidi walieleza kama ifuatavyo: -

PW1 alieleza kuwa tarehe 06/12/2021 alielezwa na msiri wake kuwa kulikuwa na namba ya Vodacom iliyokuwa ikieneza taarifa za uongo juu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo PW1 alimweleza msiri wake ampatie hiyo namba na alimpatia namba hiyo ambayo ni 0764996612. Baada ya kupata namba hiyo PW1 alimpatia PW2 hiyo namba ili afanyie uchunguzi wa kimtandao . PW2 alifanya uchunguzi wa kimtandao kwa kuangalia maeneo hiyo namba inapopatikana na kuona iko maeneo ya NMB Bariadi . PW1 na PW2 waliongozana hadi eneo la NMB na kumkamata mshtakiwa . Kabla ya kumfanyia upekuzi waliita shahidi huru aliyejulikana kwa jina la Kitwanga na walipomfanyia upekuzi huyo mshtakiwa walimkuta na simu aina ya Itel - simu janja. Ndani ya simu hiyo walikuta laini mbili za Vodacom na Tigo . Wallandika IMEI namba 355941101195986.

Baada ya kumfanyia upekuzi mtuhumiwa PW1 aliendelea kueleza kuwa walijaza hati ya upekuzi na walisaini mashahidi , maaskari wa polisi, shahidi huru na mtuhumiwa pia.

Baadae walimpeleka mtuhumiwa kituo cha polisi Bariadi na kufunguliwa kesi namba BAR/IR/2318/2021 na walimuweka mtuhumiwa chumba cha mashtaka pamoja na kielelezo cha simu . PW1 alieleza kuwa ujumbe alioandika mtuhumiwa ulisomeka kama ifuatavyo : -

"Mama yenu anakaribia kuugua ukichaa kitaalamu tunaita anachofanya hallucination. Aka kamuungano tufungeni tumuombe Mungu kavunjwe , ipo siku hawa watu wa kuvuka maji watatuingiza kwenye madeni kubwa maana wanapenda starehe kuliko kazi "

PW1 alieleza kuwa mama alimaanisha ni Mama Samia Suluhu Hassan.

PW2 aliunga mkono ushahidi wa PW1 na aliendelea kusema kuwa IMEI namba ilisajiliwa kwa jina la Hollo Yonas ambaye alipohojiwa alikiri kuwa alimpatia namba hiyo mtoto wake (mshtakiwa) aitumie lakini katika kundi la WhatsApp la Simiyu Breaking News lilionekana jina la Msenda Fatuma

PW3 alielezea Mahakama hii kuwa tarehe 06/12/2021 alipatiwa kazi na mkuu wake wa kazi ili aandike maelezo ya onyo ya mshtakiwa Levinus Kidamabi @ Tengwa . PW2 alisema baada ya kumaliza kuandaa chumba cha mahojiano na kumweleza mshtakiwa haki zake zote mshtakiwa alikataa kuletewa ndugu hivyo alitoa maelezo yake ya onyo peke yake na pia alikiri kuhusika kutenda makosa ya kutoa taarifa za uongo kwa njia ya mtandao kwenye group la WhatsApp la Simiyu Breaking News. PW3 alieleza zaidi kuwa aliscreenshot jumbe zote ndani ya simu na kuzithibitisha jumbe hizo . PW3 alitoa mahakamani caution statement (exhibit P'6') na pia karatasi zilizothibitishwa zenye jumbe za kumkashifu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na zilipokelewa Mahakamani kama vielelezo P'7' kwa pamoja.

PW4 kama mtunza stoo alieleza alikipokea kielelezo cha simu (exhibit P'2) tarehe 06/12/2021 kutoka kwa Sgt Godfrey na akakipatia namba BAR/IR/2318/2021. Baadae D/C Budodi alikichukua kwa ajili ya upelelezi na kurudisha baada ya saa moja na alikitunza . Tarehe 26/12/2021 D/C Eliakunde alichukua simu hiyo (exhibit P'2') ili aipeleke Makao Makuu ya polisi kwa uchunguzi zaidi na tarehe 29/12/2021 alirudisha simu hiyo na akaitunza stoo . PW4 alitoa

Mahakamani kielelezo cha mlolongo wa fomu ya makabidhiano (kielelezo P8).

Baada ya ushahidi wa upande wa mshtaka kutolewa mahakama hii iliona mshtakiwa ana shtaka la kujibu .

Upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi wawili ambapo mshtakiwa (DW1) alieleza mahakama hii kuwa yeye hakutenda makosa hayo na hakutoa taarifa za uongo kwani alikuwa akiwasiliana na watu wa group la WAPWA na yule waliyekuwa wakimuongelea ni kiongozi wao wa kundi hilo ambaye alitapeli au alichukua fedha kwa kudanganya wenzake kiasi cha shilingi 2,000,000/= ( milioni mbili ) kwenye akaunti yao . Alisema yeye hakumaanisha ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. DW1 alieleza alitumia simu yenye laini iliyokuwa na jina la mama yake mzazi kwa sababu aliichukua wakati akisoma chuoni .

DW2 alieleza kuwa ni kweli alimpatia mtoto wake ( mshtakiwa ) laini yake ya simu aitumie iliyokuwa na jina lake la Hollo Yonas kwa sababu wakati huo mtoto wake alikuwa akisoma chuoni

Baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili mahakama hii imeona kuwa , anayeshtaki ni lazima athibitishe .

Katika sheria ni kwamba anayedai kutendewa kosa ni lazima athibitishe na athibitishe pasipo kuacha shaka yoyote. Hii iko chini ya **Kifungu cha 3 (2) (a)** cha Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 RE 2019 ambacho kinaeleza kwamba:-

***"3 (2) (a) Katika masuala ya Jinai, isipokuwa pale ambapo sheria yoyote au sheria nyingine inatoa vinginevyo, mahakama inaridhika na upande wa mashtaka bila shaka kuwa ukweli upo".***

Msimamo wa sheria uliowekwa katika kifungu cha sheria kilichonukuliwa hapo juu umefuatwa kikamilifu na mahakama katika kesi za jinai. Katika kesi ya **Mkurugenzi wa Mashtaka V. Peter Kibatala**, Rufaa ya Jinai Na 4/2015, CAT Dar es salaam mahakama ilieleza kuwa;-

***".....wajibu wa kuthibitisha shtaka bila mashaka ya msingi ni upande wa mashtaka na mahakama ina mamlaka ya kufuta shtaka na kumwachia mshtakiwa ikiwa jukumu hilo halijatolewa".***

Huku tukiongozwa na msimamo wa sheria uliotajwa hapo juu, mahakama hii imeona kuwa upande wa mashtaka ulileta mashahidi wanne mbele ya mahakama hii kuthibitisha makosa aliyoshtakiwa mshtakiwa. Mahakama imepitia kwa makini ushahidi ulitolewa na mashahidi wa

upande wa mashtaka na upande wa utetezi kama ilivyorekodiwa katika mahakama hii.

Kutokana na ushahidi uliotolewa na pande zote mbili mahakama hii imejiuliza endapo maneno yaliyotolewa na mshtakiwa yalikua yanalenga kumdhalilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Na je, upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka yake pasi na kuacha shaka yoyote? Maneno hayo nitayaandika hapa chini :-

"Mama yenu anakaribia kuugua ukichaa kitaalamu tunaita anachofanya hallucination. Aka kamuungano tufungeni tumuombe Mungu kavunjwe, ipo siku hawa watu wa kuvuka maji watatuingiza kwenye madeni makubwa maana wanapenda starehe kuliko kazi "

" Mzazi mwenzao anawatetea wazazi wenzake "

" Mkiongozwa na mwanamke lazima mtafanywa kama wote mnanyonyesha, taifa limekuwa kama linawanawake wote, kila siku tunaongelea mambo ya kike kike "

Ukiyasoma hayo maneno hapo juu utaona kuna maneno yanayotaja "Mama", " Muungano ", watu wa kuvuka maji ", mkiongozwa na wanawake " na " mzazi mwenzao anawatetea wazazi

wenzake ". Kutokana na maneno niliyoyaandika hapo juu utaona kuwa mama ni mwanamke na katika taifa letu la Tanzania tunaongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama Samia Suluhu Hassan ambaye ni mwanamke. Yeye ni Rais anayesimamia Muungano wetu kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani ambapo lazima uvuke maji ili ufike huko Tanzania Visiwani . Pia Rais Mama Samia Suluhu Hassan alishatoa amri ya kuwarudisha wasichana wote wanaozaa kabla ya kumaliza masomo yao warudi shuleni .

Kutokana na maneno yaliyoandikwa na mshtakiwa yalikuwa yanamkashifu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani ndiye kiongozi anayeongoza serikali ya Jamhuri Muungano wa Tanzania na si kiongozi wa kundi kama alivyosema mshtakiwa kwani hana sifa ainishwa hapo juu . Pia maneno ' tuombe Mungu haka kamuungano kavunjwe ' ni maneno yaliyodhamiria kuleta uchochezi katika taifa letu . Hata hivyo mshtakiwa alikiri kwenye maelezo yake ya onyo (exhibit P '6') kuwa , **ninanukuu:-**

**"Mimi nilichangia kwa kusema mzazi mwenzao anawatetea wazazi wenzake" "Mkiongozwa na mwanamke lazima mtafanywa wote kama mnanyonyesha; Taifa**

limekuwa kama linawanawake wote. Kila siku tunaongelea mambo ya kike kike. Pamoja na hivyo watu wengine waliendelea kuchangia hoja mbalimbali na mimi niliendelea kuwajibu na tarehe 04/12/2021 saa 17:20 hrs pia niliandika ujumbe usemao "Mama yenu anakaribia kuugua ukichaa kitaalamu tunaita anachokifanya hallucination. Haka kamuungano tufungeni tumuombe Mungu kavunjwe ipo siku hawa watu wa kuvuka maji watatuingiza kwenye madeni makubwa maana wanapenda starehe kuliko kazi", hapo nilikuwa ninamaanisha mama SAMIA SULUHU HASSAN, mimi ni kweli nimetuma ujumbe mbalimbali ambao ndani yake unalenga kumbeza na kumkashifu na kutokukubali utendaji kazi wa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais SAMIA SULUHU HASSAN kwa kuwa ninaamini mawazo ya hayati Rais MAGUFULI, na siko kwenye mlengo wake Rais SAMIA yaani sifurahishwi na jinsia yake yeye kuwa Rais na Mkuu wa Nchi lakini pia sifurahishwi na mfumo wake wa uongozi"

Kutokana na uchambuzi huo hapo juu ni kweli kwamba mshtakiwa alitoa taarifa za uongo kimtandao kwa lengo la

kumkashifu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alikiri kwenye maelezo yake ya onyo na vielelezo vingine kama simu (exhibits P2) vilithibitisha taarifa hizo kutolewa na mshtakiwa. Na hakuna ubishi kuwa mshtakiwa alitumia laini ya mtu mwingine pasipo kufuata taratibu kwani yeye mwenyewe (DW1) na shahidi wake ambaye (DW2) walithibitisha hilo mahakamani. Kwa msingi huo Mahakama hii inamtia hatiani mshtakiwa kwa makosa aliyoshtakiwa nayo kama ifuatavyo:-

**Kosa la kwanza :** Uchapishaji wa Taarifa za Uongo C/S 16 ya Sheria ya Uhalifu wa kimtandao No. 14 ya 2015.

**Kosa la pili :** Uchapishaji wa Taarifa za Uongo C/S 16 ya Sheria ya Uhalifu wa Kimtandao Namba 14 ya 2015 .

**Kosa la tatu :** Kushindwa Kusajili laini ya simu iliyokuwa inamilikiwa awali na mtu mwingine kinyume na Kanuni ya 4 (1) (c), 12 (3) na 21 (1) ya Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Sim Card Registration), 2020. pamoja na Kifungu cha 152 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Na. 3 ya 2020.

## **KUMBUKUMBU ZA MAKOSA YA ZAMANI**

Hakuna rekodi za uhalifu dhidi ya mtuhumiwa lakini tunaomba mahakama imuadhibu ipasavyo mtuhumiwa na hii itakuwa fundisho kwa watumiaji wengine wa mitandao ya kijamii.

## **SHUFAA ZA MSHTAKIWA**

Naomba mahakama inionee huruma kwani ndio kwanza nimetenda makosa haya na nina familia inayonitegemea.

## **SENTENSI**

Mtuhumiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza. Kwa kuzingatia yote hayo

Mahakama inamhukumu mtuhumiwa kama ifuatavyo:-

**Kosa la Kwanza:** Mshtakiwa alipe faini ya Tsh . 5,000,000/= na kifungo cha miaka mitatu jela.

**Kosa la pili:** Mshtakiwa alipe faini ya Tsh . 5,000,000/= na kifungo cha miaka mitatu jela.

**Kosa la tatu:** Mshtakiwa alipe faini ya Tsh . 5,000,000/= na kifungo cha mwaka mmoja.

Hukumu ya kifungo itaenda sambamba.

Imeamriwa hivyo.

**M. J. MAHUMBUGA - PRM**

**19/10/2022**

Haki ya kukata rufaa imeelezwa.



**M. J. MAHUMBUGA - PRM**

**19/10/2022**

Mshakiwa arudishiwe simu yake iliyotolewa kama kielelezo hapa  
maha. marir.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI  
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI  
SIMIYU.

**M. J. MAHUMBUGA - PRM**

**19/10/2022**